



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS



**BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA
MAZINGIRA**

**MKUTANO WA WADAU JUU YA KATAZO LA MATUMIZI YA MIFUKO YA
PLASTIKI UTAKAOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA
KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE (JNICC) TAREHE 14 APRILI, 2023
SAA 3:00 ASUBUHI.**

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam wameandaa Mkutano juu ya Katazo la Matumizi ya Mifuko ya Plastiki kwa Wazalishaji, Wazambazaji, Waingizaji na Wadau wengine utakaofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) tarehe 14 aprili, 2023.

Lengo la Mkutano huo ni kukuza uelewa juu ya matakwa ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Kupiga Marufuku Mifuko ya Plastiki) za mwaka 2022. Mgeni rasmi katika Mkutano huo ni Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, CPA Amosi G. Makalla.

Hivyo, wadau wote mnaalikwa kushiriki Mkutano huu muhimu utakaotoa fursa ya kuainisha changamoto mbalimbali na kutoa maoni juu ya namna bora ya kuimarisha Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni.

*Imetolewa na Mkurugenzi Mkuu
Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira
12 Aprili, 2023*